
OFISI YA RAIS

UTUMISHI

NA UTAWALA BORA



TOLEO LA MACHI- 2025

YALIYOMO

1	WAZIRI SIMBACHAWENE: e-GA IMEFANIKIWA KUJENGA MFUMO WA KUBADILISHANA TAARIFA KWENYE TAASISI ZA SERIKALI	1
2	MHE. SANGU: WARUDISHENI KAZINI WATUMISHI WALIOSHINDA RUFAA	4
3	WAZIRI SIMBACHAWENE ASHIRIKI IBADA YA SHUKRANI YA ALIYEKUWA WAZIRI MKUU, HAYATI EDWARD LOWASSA, ASISITIZA SUALA LA AMANI	5
4	OFISI YA RAIS-UTUMISHI YAZINOA TAASISI ZA MALIASILI NA UTALII KUANDAA DAFTARI LA HUDUMA ZA SERIKALI	7
5	STORI ZA BUNGE	9
6	WAZIRI SIMBACHAWENE AIPONGEZA MENEJIMENTI YA OFISI YAKE KUBUNI SIKU MAALUM “UTUMISHI DAY GALA”, ASISITIZA ITUMIKE KUWAKUMBUSHA WATUMISHI KUTIMIZA WAJIBU	11
7	KAMATI YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA YAIPONGEZA SEKRETARIETI YA AJIRA	14
8	WAELIMISHA RIKA OFISI YA RAIS-UTUMISHI WATAKIWA KUTOA ELIMU KUHUSU UIMARISHAJI WA AFYA KWA WATUMISHI	16
9	WAZIRI WA UTUMISHI ZANZIBAR MHE. HAROUN ASISITIZA MASHIRIKIANO BAINA YA SJMT NA SMZ KATIKA MASUALA YA UTUMISHI	18
10	OFISI YA RAIS-UTUMISHI YAPATIWA ELIMU YA KINGA NA TAHADHARI DHIDI YA MAJANGA YA MOTO	20
11	NAIBU KATIBU MKUU, DAUDI ATAJA SABABU ZA WANACHI KUTOKUTUMIA MFUMO RASMI WA KUWASILISHA MALALAMIKO SERIKALINI	22
12	NENDENI MKALETE MAPINDUZI KATIKA MADAWATI YA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO YA WANANCHI - MKURUGENZI LEILA MAVIKA	24
13	WAZIRI SIMBACHAWENE ATOA MAAGIZO KUMI YA KIMKAKATI KWA WAKUU WA IDARA ZA UTAWALA NA USIMAMIZI WA RASILIMALIWATU SERIKALINI	26
14	MAELEZO YA HABARI KATIKA PICHA	30



1

WAZIRI SIMBACHAWENE: e-GA IMEFANIKIWA KUJENGA MFUMO WA KUBADILISHANA TAARIFA KWENYE TAASISI ZA SERIKALI

Na Lusungu Helela - ARUSHA

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene amesema Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imefanikiwa kujenga mfumo ambao unawezesha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) Serikalini kuunganishwa, kuwasiliana na kubadilishana taarifa.

Amesema kwa sasa mifumo 218 kutoka kwenye Taasisi zipatazo 181 imeunganishwa na inasomana.

Amesema hatua hiyo imekuja kufuatia kuitikia agizo la Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan la kutaka mifumo inayotumika kwenye Taasisi za Umma kusomana ili kurahisisha utendaji kazi Serikalini na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mhe. Simbachawene ameyasema hayo hivi karibuni jijini Arusha wakati Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Philip Mpango akifungua Kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao kwa niaba ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Amesema e-GA itaendelea kusimamia uunganishwaji wa mifumo ya kubadilishana taarifa kulingana na mahitaji yaliyopo.

Aidha, Mhe. Simbachawene amesema kikao kazi hicho kilimualika Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa lengo la kumshukuru kwa mchango wake mkubwa pamoja na kutoa hamasa katika matumizi ya TEHAMA kwani ndiyo chachu iliyopelekea mafanikio hayo yanayoonekana kitaifa na kimataifa.

Katika hatua nyingine, Mhe. Simbachawene amesema Tanzania imeweza kutambulika Duniani kwa kushika nafasi ya pili katika Bara la Afrika na kuwa ya kwanza katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kwenye ripoti ya utafiti wa ukomavu wa matumizi ya teknolojia katika kutoa huduma za Serikali na ushirikishwaji wa wananchi kulingana na ripoti ya Benki ya Dunia.

Ameongeza kuwa “Kama nchi tumepiga hatua kubwa katika uwezo wa kujenga miundombinu ya kuhifadhi taarifa na kuweza kubadilisha utendaji kazi wetu kwenda kwa njia ya mtandao"

Awali Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, (e-GA) Mhandisi Benedict Ndomba alisema e-Ga imesaidia matumizi sahihi na ya uhakika kwenye Taasisi za Serikali kwa kuwezesha utoaji wa huduma kwa wakati.

Amesema e-GA imeleta mapinduzi makubwa katika matumizi ya TEHAMA Serikalini kwani imechagiza utendaji kazi wa Serikali na kuongeza ufanisi kwenye Taasisi mbalimbali ikiwemo Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) Mifumo ya fedha ya Benki Kuu (BOT) pamoja na Mfumo wa Manunuzi (Nest).

Naye Katibu Mkuu-IKULU, Bw. Mululi Mahendeka amesema e-GA imeleta mageuzi makubwa kwenye Taasisi za Serikali kwa kuboresha utendaji kazi wa kila siku na utoaji wa huduma kwa jamii kuwa rahisi na wa haraka.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Joseph Mhagama amesema Bunge ni moja ya wanufaika wakubwa wa gunduzi zilizofanywa na e-Ga.

Amesema Serikali imepiga hatua kubwa kwenye matumizi ya mifumo ya TEHAMA ambayo yameleta tija na ufanisi wa hali ya juu latika utoaji wa huduma bora za haraka na za uhakika kwa wananchi.

"Tunaipongeza sana e-GA kwa bunifu wanazoendelea kufanya, kama Bunge tunataka mifumo yote ya kidigitali inayotumika na Serikali isimamiwe na idhibitiwe na e-GA ili kulinda taarifa za Serikali.



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Philip Mpango akiwa ameongozana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene wakati wa ufunguzi wa Kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao kinachofanyika kwa muda wa siku tatu jijini Arusha



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango akizungumza kwa niaba ya Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa ufunguzi wa Kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao kinachofanyika kwa muda wa siku tatu jijini Arusha.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akizungumza kabla ya kumkaribisha Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango kuzungumza kwa niaba ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa ufunguzi wa Kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao kinachofanyika kwa muda wa siku tatu jijini Arusha






Sehemu ya Washiriki wa kikao kazi cha 5 cha Serikali Mtandao kinachofanyika kwa muda wa siku tatu jijini Arusha kilichofunguliwa leo na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango kwa niaba ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan

2

MHE.SANGU : WARUDISHENI KAZINI WATUMISHI WALIOSHINDA RUFAA



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Sangu akizungumza wakati akifungua mafunzo kuhusu Mfumo wa ushughulikiaji wa Rufaa na Malalamiko katika Utumishi wa Umma yanayofanyika hivi karibuni mkoani Morogoro.

Na Mwandishi Wetu - Morogoro

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imewataka Waajiri wa taasisi za umma kuwarudisha kazini watumishi wanaoshinda mashauri ya rufaa za kinidhamu kadiri ya maelekezo yaliyotoka kwenye Tume ya Utumishi wa Umma

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Mhe. Deus Sangu ametoa agizo hilo akiwa Morogoro katika hotuba yake ya ufunguzi wa kikao kazi kuhusu mafunzo ya matumizi ya mfumo wa kieletroniki wa kushughulikia rufaa na malalamiko na Ukaguzi wa Usimamzi wa Masuala ya Rasilimali Watu (PSCMIS) yaliyoandaliwa na tume hiyo.

Mhe. Sangu amesema kuna baadhi ya viongozi wa taasisi za umma ambazo majina yake ameyahifadhi kuwa wamekaindi maelekezo ya tume hiyo na itabidi wachukuliwe hatua zinazostahiki,

Naibu Waziri Mhe. Sangu amesema kwenye ziara zake aliyoifanya mikoani amekutana na watumishi wakiwa na wana barua halali zilizowaarejesha kazini kutoka Tume ya Utumishi wa Umma.

"Kuna baadhi ya waajiri hawajawarudisha watumishi kazini,watumishi hao wameandikiwa barua na hawajawarudisha na huu ni mwaka wanne sitazitaja taasisi hizo lakini zipo kama tano wamewagomea watumishi wale."



3

WAZIRI SIMBACHAWENE ASHIRIKI IBADA YA SHUKRANI YA ALIYEKUWA WAZIRI MKUU, HAYATI EDWARD LOWASSA, ASISITIZA SUALA LA AMANI

Na Mwandishi Wetu - Monduli

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene amewataka Watanzania kumuenzi aliyekuwa Waziri Mkuu, Hayati Edward Lowassa kwa kuendelea kudumisha umoja, amani na mshikamano ili kuepuka mapigano yanayoendelea katika nchi zingine.

Mhe. Simbachawene ametoa kauli hiyo leo hiyo hivi karibuni wakati wa Ibada maalumu ya Kumbukizi ya mwaka mmoja wa aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania, Hayati Edward Lowassa huku akiwataka Watanzania kuendeleza yale yote mazuri aliyokuwa akiyafanya.

Aidha, Mhe. Simbachawene amesema Hayati Edward Lowassa atakumbukwa daima kwa kuwagusa watu wengi kwa namna chanya.

Amefafanua kuwa Hayati Edward Lowassa ni Kiongozi aliyekuwa na upendo, aliyewasaidia watu wengi na aliyependa kuzungumza na kila mtu bila kujali anamfahamu au hamfahamu.

Ameongeza kuwa "Hayati Edward Lowassa ni kiongozi aliyekuwa hapendi kumuona mtu yeyote akipata shida, alitamani kumuona kila mmoja akiwa na furaha wakati wote" amesema.

Katika hatua nyingine Mhe. Simbachawene amemshukuru Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kumuenzi Hayati Lowassa kwa mchango wake chanya aliokuwa akiutoa kwa maendeleo ya Taifa.

“Hivi sasa tuna shule nyingi zimejengwa na zimeendelea kujengwa, barabara, miradi ya maji imeendelea kutekelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan” ameongeza.

Akizungumza kwa niaba ya Familia ya Hayati Edward Lowassa, mtoto wa kwanza ambaye pia ni Mbunge wa Monduli, Mhe. Fredrick Lowassa ametumia fursa hiyo kuwashukuru wote waliokuwa pamoja tangu baba yao alipofariki hadi hivi sasa huku akimtaja Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mchango wake mkubwa kwa familia hiyo tangu baba yao alipoanza kuugua hadi umauti ulipomkuta.

"Ikiwa leo ni mwaka mmoja tangu baba yetu atutoke, alikuwa ni kiongozi na nembo ya Wananchi wa Monduli, tuendelee kumuenzi kwa mchango wake mkubwa katika kudumisha mshikamano kwa jamii za wafugaji wa asili" amesisitiza Mhe. Fredrick Aidha, Ametumia fursa hiyo kuiomba Serikali iharakishe mchakato wa kuandaa Makumbusho ya Hayati Edward Lowassa kutokana na ujio wa wageni wengi wanaofika nyumbani hapo kwa ajili ya kujifunza mambo aliyokuwa akiyafanya baba yao.

Naye, Baba Askofu Mstaafu wa Kanisa la Kiinjili la kilutheri Tanzania KKKT Dayosisi ya Kaskazini Kati, Dkt. Solomon Masangwa ameisisitiza familia ya Hayati Edward Lowassa kuzidi kumshirikisha Mungu katika kila jambo wanalolifanya ili kuendelea kushikamana.

Hayati Edward Ngoyai Lowassa alifariki dunia Februari 10, 2024 na kuzikwa nyumbani kwake Monduli tarehe 17 Februari 2024.



Sehemu ya wanafamilia wa Hayati Edward Lowassa wakiwa kwenye Ibada ya Shukrani ya aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu, Hayati Edward Ngoyai Lowassa iliyofanyika leo katika Kanisa la Kiinjili Kilutheri Tanzania (KKKT) Monduli Mjini Mkoani Arusha.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akizungumza katika Ibada ya Shukrani ya aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu Hayati Edward Ngoyai Lowassa iliyofanyika katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Monduli Mjini Mkoani Arusha.

4 OFISI YA RAIS-UTUMISHI YAZINOA TAASISI ZA MALIASILI NA UTALII KUANDAA DAFTARI LA HUDUMA ZA SERIKALI



Na Lusungu Helela - Dodoma

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeanza kuwanoa Watumishi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu kuandaa Daftari la kielektroniki la Huduma za Serikali kwa Taasisi zote za Serikali kwa lengo la kuwawezesha wananchi na wadau mbalimbali kupata taarifa za huduma zote zinazotolewa na Taasisi za Serikali kwenye chanzo kimoja.

Hayo yamesemwa jijini Dodoma na Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - UTUMISHI, SACP. Ibrahim Mahumi wakati akifungua kikao kazi kuhusu Daftari la Huduma za Serikali kilichowakutanisha baadhi ya Watumishi kutoka Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii,

SACP Mahumi amesema Daftari hilo ni muendelezo wa utengenezaji wa mifumo ya kuiwezesha serikali kutoa huduma bora kwa wananchi.

Kufuatia hatua hiyo SACP. Mahumi amewataka Watumishi hao kuzingatia mafunzo ya uandaaji wa daftari hilo kwani litakuwa chachu ya kuboresha utoaji wa huduma katika Taasisi za Wizara hiyo.

Amewasihi Watumishi hao kutambua kuwa Mteja ndiyo mlengwa mkuu wa daftari hilo hivyo wahakikishe huduma zote zinazotolewa na Taasisi zao zinaainishwa na kuingizwa kwenye daftari hilo kwa usahihi wa hali ya juu.

Akitolea mfano wa Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) SACP. Mahumi amesema ili Mwananchi aweze kupata huduma katika taasisi hiyo ni lazima awe na taarifa za kutosha kwa kuzingatia huduma zinazotolewa, gharama na muda utakaotumika kupata huduma hizo.

Katika hatua nyingine, SACP. Mahumi amewataka washiriki wa mafunzo hayo wakawe mabalozi na wakatumie muda kuwafundisha watumishi wengine ili waweze kujua umuhimu wa daftari hilo.

Awali, Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Bw. Patrick Marcelline, ameushukuru uongozi wa Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mafunzo hayo muhimu, na kuahidi kuwa Wizara itayatumia Mafunzo hayo kama nyenzo muhimu ya kuboresha huduma zake kwa maslahi mapana ya Uhifadhi na Utalii na Taifa kwa ujumla

Kikao kazi hicho cha siku tatu cha uandaaji wa Daftari la Huduma za Serikali kinawezeshwa na timu ya wataalam wabobezi kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.



Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI, SACP.Ibrahim Mahumi akiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya Watumishi kutoka Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii mara baada kufungua kikao kazi kuhusu uandaaji wa Daftari la Huduma za Serikali



Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI, SACP.Ibrahim Mahumi akizungumza wakati akifungua kikao kazi kuhusu uandaaji wa Daftari la Huduma za Serikali kilichowakutanisha baadhi ya Watumishi kutoka Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii



Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI, SACP. Ibrahim Mahumi akisalimiana na Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wa kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Bw. Patrick Marcelline mara baada ya kuwasili kwa ajili ya kuzungumza na Watumishi wakati akifungua kikao kazi kuhusu uandaaji wa Daftari la Huduma za Serikali

5 KUTOKA BUNGENI:

SERIKALI YAZIDI KUWAPANDISHA VYEO MAELFU YA WATUMISHI

Serikali imesema kwamba katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 imewapandisha vyeo watumishi 180,000 wakiwemo watumishi walioathirika na mwongozo wa upandaji madaraja wa miaka minne.

Mhe. Sangu amesema hayo wakati akijibu swali la Janejelly Ntate (Viti Maalumu) aliyetaka kujua Serikali imejipangaje kukwamua watumishi walioathiriwa na mwongozo wa upandaji madaraja wa miaka minne.

Aidha, katika utekelezaji wa Ikama na Bajeti ya Mwaka 2023/2024, Serikali imewapandisha vyeo watumishi zaidi ya 232,530 wakiwemo walioathirika na zoezi hilo, uhakiki wa vyeti feki na watumishi hewa.

WAZIRI MHE.SANGU : MFUMO WA UPIMAJI UTENDAJI KUJAZWA KILA WIKI NA WATUMISHI NA SIO VINGINEVYO

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Sangu amesema Mfumo wa upimaji wa utendaji kazi kwa Watumishi wa Umma ujulikanao kama PEPMIS utaendelea kujazwa kwa wiki kama ilivyopangwa.

Mhe. Deus Sangu amesema hayo Bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu, Mhe. Sophia Mwakagenda aliyetaka kujua kwa nini watumishi wa afya wasijaze ripoti za utendaji kila mwezi badala ya kila wiki ili wapate muda zaidi kuhudumia wagonjwa.



NAIBU WAZIRI SANGU AWATAKA WAAJIRI KUJA NA MKAKATI WA MAFUNZO KWA WATUMISHI WA UMMA

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi.wa Umma na Utawala Bora, Mhe.Deus Sangu amesema katika kuhakikisha Watumishi wa Umma wanaendelezwa katika taaluma zao ili kuendana na kasi ya maendeleo na kuongeza ufanisi, waajiri wote.

wanapaswa kuainisha mahitaji ya mafunzo, kuandaa mipango ya mafunzo na kutenga bajeti kila mwaka na kusimamia utekelezaji wake.

"Serikali imekuwa ikipokea fursa za mafunzo ya muda mrefu na mfupi kutoka maeneo mbalimbali ya kimkakati kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo wakiwemo Korea Kusini, China, India, Indonesia, Japan, Singapore, Misri, Malaysia, Thailand,Bangladesh ambapo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 zaidi ya watumishi 1,278 walinufaika na fursa hizo" - amesema Mhe. Sangu.

Mhe.Sangu ameyasema hayo Bungeni Dodoma hivi karibuni wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Iringa, Mhe.Nancy Nyalusi kuhusiana na mpango wa Serikali wa kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Umma ili kuendana na kasi ya maendeleo ili kuongeza ufanisi

NAIBU WAZIRI SANGU : TASAF IMESAIDIA KUBORESHA MAISHA YA WANANCHI ZANZIBAR

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejiment ua Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.Deus Sangu amesema kupitia tathmini ya Kipindi cha Kwanza cha Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini iliyokamilika mwaka 2019 ilionesha kwamba mpango wa kunusuru kaya maskini Zanzibar kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) imeonesha maendeleo makubwa kwa wananchi wakiwemo wa Zanzibar.

Ameyasema hayo wakati akijibu swali la Mbunge wa Jimbo la Amani (Zanzibar), Mhe. Abdul Yussuf Maalim, aliyetaka kujua tathmini ikoje juu ya maendeleo ya kaya maskini zilizodhaminiwa na TASAF kwa upande wa Zanzibar.

Mhe. Sangu amesema tathmini ya kipindi cha pili itakamilika mwezi Juni, 2025 huku akisema walengwa wanapata mahitaji ya msingi kama vile chakula na vifaa vya shule kwa watoto pamoja na makazi ya kuishi kuboreshwa.

Pia Mhe.Sangu ametaja mafanikio mengine ikiwa ni kuongezeka kwa mahudhurio ya watoto katika Skuli kufikia asilimia 95 na pia viwango vya ufaulu vimeongezeka na kwamba wazazi pia wameweza kupeleka watoto kliniki kwa zaidi ya asilimia 95 kwa ajili ya ushauri wa kitaalamu na kuongezeka kwa mzunguko wa fedha miongoni mwa wananchi na kuchochea ukuaji wa shughuli za uchumi katika maeneo hayo ya visiwa vya Unguja na Pemba.

6 WAZIRI SIMBACHAWENE AIPONGEZA MENEJIMENTI YA OFISI YAKE KUBUNI SIKU MAALUM “UTUMISHI DAY GALA” ASISITIZA ITUMIKE KUWAKUMBUSHA WATUMISHI KUTIMIZA WAJIBU



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe.George Simbachawene ameipongeza menejimenti ya Ofisi yake kwa kuwa wabunifu katika masuala mbalimbali ya kiutumishi ikiwemo kubuni tukio la "Utumishi Day Gala”.

Mhe. Simbachawene ametoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki hii jijini Dodoma katika Siku maalum ya "Utumishi Day Gala 2025” iliyoandaliwa na menejimenti ya Ofisi yake kwa lengo la kubadilishana uzoefu ili kuboresha utendaji kazi hasa katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Amesema Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora itabaki kuwa Ofisi Kiongozi kutokana na bunifu mbalimbali ambazo imekuwa ikifanya kwa lengo la kuhakikisha Watumishi wake wanakuwa vinara wa kutoa huduma bora kwa wananchi.

Ameongeza kuwa Ofisi hiyo imekuwa ikijipambanua katika masuala mbalimbali ambayo huwezi kukutana

nayo katika Wizara yeyote isipokuwa Utumishi lengo likiwa ni kuhakikisha Watumishi wanajengewa mazingira bora na wezeshi katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Amesema utamaduni huo wa kukutana mara moja kwa kila mwaka unatoa motisha kwa watumishi na kuongeza ufanisi na uwabikaji katika kutekeleza majukumu yao

Mhe. Simbachawene amesisitiza kuwa ni vema siku hiyo maalum ikatumika kuhamasisha na kuwakumbusha watumishi wa Ofisi hiyo kutimiza wajibu wao kwa kutoa huduma bora kwa wananchi kwani wananchi wakihudumiwa kwa furaha, amani na utumilivu vinatawala nchini.

" Nimebahatika kuwa Waziri katika Wizara tisa lakini huu utamaduni wa kukutana kwa pamoja kama leo hii tulivyokutana hapa tunafurahi kwa pamoja haikuwahi kutokea, hakika hili jambo linapaswa kuigwa na Wizara zingine" alisisitiza Mhe.Simbachawene

Ameongeza kuwa " Unaweza kudhani umeshaona mambo yote kumbe hapana hili la "Utumishi Day Gala" kwangu mimi ni jipya hakika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni Ofisi Kiongozi katika nyanja zote na ndivyo inavyotakiwa, hongereni sana Menejimenti kwa ubunifu huu".

Naye Naibu Waziri wa Ofisi hiyo Mhe. Deus Sangu ametumia fursa hiyo kuipongeza timu ya Menejimenti kwa wazo hilo la "Utumishi Day Gala" huku akiwataka Watumishi kufurahia huku wakibadilisha mbinu za kuhakikisha kila mmoja anakuwa kinara wa kutoa huduma bora kwa wananchi.

Awali Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi amesema tukio hilo hufanyika mara moja kila mwaka ambapo Watumishi hukutana kwa pamoja ikiwa ni fursa adhimu kwao kutokana majukumu mengi wanayoyatekeleza kuwapelekea kutokuonana kwa pamoja kama ilivyo kwa "Utumishi Day Gala"

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akizungumza na watumishi wa ofisi yake kwenye Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma katika siku maalum (UTUMISHI DAY GALA 2025) iliyoandaliwa na Menejimenti ya ofisi yake kwa lengo la kujenga umoja na kuongeza chachu ya utendaji kazi.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Sangu (kulia) akifurahia jambo na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi (kushoto) katika siku maalum (UTUMISHI DAY GALA 2025) iliyoandaliwa na menejimenti ya ofisi hiyo jijini Dodoma kwa lengo la kujenga umoja na kuongeza chachu ya utendaji



Baadhi ya Watumishi wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI waliohudhuria katika siku maalum (UTUMISHI DAY GALA 2025) iliyoandaliwa na menejimenti ya ofisi hiyo kwa lengo la kujenga umoja na kuongeza chachu ya



Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi akitoa neno la utangulizi kabla ya kumkaribisha Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (hayupo pichani) kuzungumza na watumishi wa ofisi hiyo katika siku maalum (UTUMISHI DAY GALA 2025) iliyoandaliwa kwa lengo la kujenga umoja na kuongeza chachu ya utendaji kazi kwa watumishi



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Sangu akizungumza na watumishi wa ofisi yake jijini Dodoma katika siku maalum (UTUMISHI DAY GALA 2025) iliyoandaliwa na Menejimenti ya ofisi hiyo kwa lengo la kujenga umoja na kuongeza chachu ya utendaji kazi kwa watumishi wa ofisi yake.

7

KAMATI YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA YAIPONGEZA SEKRETARIETI YA AJIRA

Na Mwandishi Wetu — DODOMA

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria imeipongeza Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kuhakikisha michakato ya ajira inafanyika kwa ufanisi na kwa uwazi wa hali ya juu.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo , Mhe. Dkt. Joseph Mhagama ametoa pongezi hizo hivi karibuni jijini Dodoma kwa niaba ya Kamati yake wakati wa kikao kazi cha kamati hiyo na Watendaji wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kilicholenga kupokea na kujadili taarifa ya utendaji kazi ya mwezi Septemba 2024 hadi Januari 2025.

Mhe. Dkt. Mhagama mesema kitendo cha ya kuwalazimu waombaji kazi wote kufika jijini Dodoma kumeleta ahueni kubwa kwa waombaji kazi hao hususani wale waliotoka kwenye familia maskini.

Hapo awali wazazi walilazimika kuuza ardhi au ngombe ili kijana wao aweze kusafiri kuja jijini Dodoma kwa ajili ya kufanya usaili ila ubunifu wa kufanya usaili kimkoa umerahisishia. Amesema Mhe. Dkt. Mhagama amesema

Amesisitiza kuwa utaratibu huo umeondoa usumbufu pamoja na kumfanya Muombaji kazi kutokutumia gharama ya usafiri kwa ajili ya kufika jijini Dodoma kufanya usaili.

Akizungumzia matumizi ya mfumo wa Ajira Portal kwa waombaji kazi Mhe.Dkt. Mhagama amesema mfumo juo umeondoa dhana ya upendeleo wa kupata ajira katika Utumishi



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akijibu hoja zilizotolewa na Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria mara baada ya Wajumbe hao kupokea na kujadili taarifa ya utendaji kazi wa Ofisi ya Rais, UTUMISHI na Utawala Bora

wa Umma na kuchagiza ushindani miongoni mwa waombaji kwani hutoi fursa ya kuonana ana kwa ana na wahusika

Nimekuwa nikipokea simu nyingi kutoka kwa Watoto wa familia masikini wa kutoka vijijini wakiwa wamepata ajira serikalini pasipo kumjua yeyote aliyepo serikalini amesisitiza Mhe. Dkt. Mhagama.

Kwa Upande wake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene amesema ajira katika Utumishi wa Umma zinapatikana kwa ushindani kutokana na idadi kubwa ya wasomi iliyopo lakini nafasi ni chache

Ametumia fursa hiyo kuwaomba Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa Mabalozi wa Sekretariet ya Ajira Katika Utumishi wa Umma kwa kuwaeleza wananchi kuwa ajira katika Utumishi wa Umma hazihitaji kumjua yeyote na cha msingi ni kufuata taratibu zilizowekwa na Sekretarieti hiyo wakati wa kuomba kazi.



Mwenyekiti wa Kamati ya ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria , Mhe. Dkt. Joseph Mhagama akizungumza na Wajumbe mara baada ya Naibu Waziri Mhe. Deus Sangu kuwasilisha taarifa ya utendaji kazi wa Ofisi ya Rais, UTUMISHI na Utawala Bora kwa niaba ya Waziri Mhe.



Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria wakimsikiliza Naibu Waziri Mhe. Deus Sangu mara baada ya kupokea na kujadili taarifa ya utendaji kazi wa Ofisi ya Rais, UTUMISHI na Utawala Bora kwa niaba ya Waziri Mhe. George

8 WAELIMISHA RIKA OFISI YA RAIS-UTUMISHI WATAKIWA KUTOA ELIMU KUHUSU UIMARISHAJI WA AFYA KWA WATUMISHI



Sehemu ya Waelimisha Rika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, wakifuatilia mafunzo yaliyolenga kuwajengea uwezo Waelimisha Rika wa Idara na Vitengo vya ofisi hiyo ili kupambana na Afua za VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza mahali pa kazi yaliyofanyika katika ofisi hiyo iliyopo Mji wa Serikali Mtumba.

Na Veronica Mwafisi - Dodoma

Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Uendelezaji Sera, Sehemu ya Anuai za Jamii, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bi. Mwanaamani Mtoo ametoa wito kwa Waelimisha Rika wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI kutoa elimu kwa watumishi walio kwenye Idara na Vitengo vya Ofisi hiyo namna ya kutunza na kuimarisha afya ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kwa masilahi mapana ya taifa.

Bi. Mtoo ametoa wito huo jijini Dodoma wakati akifungua mafunzo yaliyotolewa kwa Waelimisha Rika hao yaliyolenga kuwajengea uwezo katika kutekeleza majukumu yao.

Amesema kuwa Waelimisha Rika katika ofisi ni watu muhimu hivyo mafunzo hayo yatawasaidia kufahamu mbinu mbalimbali za kutumia katika utoaji wa elimu na namna ya kuimarisha afya za watumishi wenzao ili ziwasaidie katika kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa kuzingatia utunzaji ya afya bora.

“Ninyi ni watu muhimu sana katika ofisi zetu, naamini mafunzo haya yatawajengea uwezo mkubwa wa kutoa elimu na kuwaelekeza watumishi wenzenu namna ya kutunza na kuimarisha afya iliyo bora, na hapa niwakumbushe kuzingatia lishe iliyo bora ili muweze kutekeleza majukumu ya taifa,” Bi. Mtoo amesema.

Akiwasilisha mada kuhusu lishe bora, Afisa Lishe kutoka Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma,

, Bi. Nusrat Rubambura amesisitiza masuala ya kuzingatia katika kuimarisha afya ikiwemo kufanya mazoezi, kunywa maji ya kutosha pamoja na kula vyakula mchanganyiko kutoka katika makundi sita ikiwemo nafaka, mizizi na ndizi za kupika, asili ya wanyama, jamii ya kunde, mbogamboga, matunda na Mafuta salama.

Akizungumza kwa niaba ya Waelimisha Rika hao, Mwenyekiti wa Waelimisha Rika Bw. Kokolo Lusanda ameahidi watashirikiana katika kutoa elimu kwa watumishi wenzao ili kuzingatia utunzaji wa afya zao na kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.



Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Uendelezaji Sera, Sehemu ya Anuai za Jamii, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bi. Mwanaamani Mtoo akisisitiza jambo wakati akifungua mafunzo yaliyolenga kuwajengea uwezo Waelimisha Rika wa Idara na Vitengo vya ofisi hiyo ili kupambana na Afua za VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza mahali



Sehemu ya Waelimisha Rika, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, wakimsikiliza Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Uendelezaji Sera, Sehemu ya Anuai za Jamii, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bi. Mwanaamani Mtoo (hayupo pichani) wakati akifungua mafunzo yaliyolenga kuwajengea uwezo Waelimisha Rika wa Idara na Vitengo vya ofisi hiyo ili kupambana na Afua za VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza mahali pa kazi.

9

WAZIRI WA UTUMISHI ZANZIBAR MHE. HAROUN ASISITIZA MASHIRIKIANO BAINA YA SJMT NA SMZ KATIKA MASUALA YA UTUMISHI

Na Veronica Mwafisi

Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Haroun Ali Suleiman amewataka Wakurugenzi kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (SJMT) na Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (SMZ) kuendeleza mashirikiano katika masuala ya utumishi kwa ustawi wa maendeleo ya taifa.

Mhe. Suleiman amesema hayo wakati akihitimisha kikao kilicholenga kuimarisha ushirikiano katika masuala ya kiutumishi baina ya ofisi hizo mbili kilichofanyika kwa siku tatu jijini Dodoma.

Mhe. Suleiman amesema kikao hicho kiongeze tija katika utendaji kazi ikiwemo kubadilishana uzoefu kuhusu masuala mbalimbali ya kiutumishi pamoja na kujadili changamoto mbalimbali zitakazosaidia kuimarisha utumishi kwa ufanisi mkubwa kwa maendeleo ya taifa.

Aidha, Waziri Suleiman amewataka washiriki wa kikao hicho kuwa wazalendo, waaminifu na waadilifu, kusimamia walio chini yao na kutii maagizo ya viongozi walio juu yao.

Kwa Upande wake, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Mhe. Deus Sangu akimwakilisha Waziri wa Ofisi hiyo, Mhe. George Simbachawene amesema kikao hicho kitawajengea uwezo mkubwa katika kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa kuzingatia miongozo na kanuni za Utumishi wa Umma.

Awali, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi amesema kikao hicho kitasaidia kuimarisha mashirikiano mazuri baina ya ofisi hizo mbili na kuahidi kuendelea kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa majukumu kwa masilahi mapana ya nchi.

Katika Kikao hicho cha siku tatu moja ya maazimio yaliyopitishwa ni kutoa pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa



Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Haroun Ali Suleiman (aliyevaa tai nyeusi) akiwasili katika eneo la kikao kilichofanyika baina ya Ofisi ya Rais-UTUMISHI na Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (SMZ) kilicholenga kuimarisha ushirikiano katika masuala ya kiutumishi.



Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Haroun Ali Suleiman (kushoto) akizungumza wakati wa kikao baina ya Ofisi ya Rais-UTUMISHI na Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (SMZ) kilicholenga kuimarisha ushirikiano katika masuala ya kiutumishi kilichofanyika jijini Dodoma.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akizungumza katika Ibada ya Shukrani ya aliyekuwa Waziri Mkuu Mstaafu Hayati Edward Ngoyai Lowassa iliyofanyika katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Monduli Mjini Mkoani Arusha.

10 OFISI YA RAIS-UTUMISHI YAPATIWA ELIMU YA KINGA NA TAHADHARI DHIDI YA MAJANGA YA MOTO



Baadhi ya Wakurugenzi na Watumishi wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI wakimsikiliza Mrakibu Msaidizi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Bw. Iddi Chanyika (kulia) wakati akifafanua jambo kwenye mafunzo ya uelewa kuhusu kuchukua tahadhari dhidi ya majanga ya moto yaliyofanyika katika ofisi hiyo iliyopo Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma.

Na Veronica Mwafisi - Dodoma

Watumishi wa Ofisi ya Rais-UTUMISHI wameaswa kuchukua tahadhari dhidi ya majanga ya moto pamoja na matumizi sahihi ya namba ya dharula 114 ili kutunza jengo la ofisi hiyo na kuendelea kutoa huduma kwa wateja wanaofika ofisini hapo bila kuwa na shaka yoyote.

Wito huo umetolewa na Mrakibu Msaidizi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Bw. Iddi Chanyika wakati wa mafunzo kwa watumishi wa ofisi hiyo yanayotolewa kila Jumatatu ya wiki kwa lengo la kujenga uelewa wa masuala ya kiutumishi ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Bw. Chanyika ameeleza kuwa, Ofisi ya Rais-UTUMISHI inapokea wateja wengi kwa ajili ya kupata huduma mbalimbali za kiutumishi hivyo, ili kulinda usalama wa wateja wanaoingia na kutoka kwa ajili ya kupata huduma hizo ni muhimu kuchukua tahadhari hasa katika kuangalia usalama wa jengo la ofisi hiyo.

Aidha Bw. Chanyika ameipongeza Ofisi ya Rais-UTUMISHI kwa kuwa na vifaa mbalimbali vya tahadhari kwa ajili ya kujikinga na madhara ya moto yanayoweza kutokea.

“Niipongeze ofisi hii kwa kuzingatia usalama wa jengo kwani nimeona mna vifaa kwa ajili ya tahadhari dhidi ya moto vikiwemo ving’amua moto,” amesema Bw. Chanyika.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mipango, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Cosmas Ngangaji ametoa shukrani kwa niaba ya Watumishi wa ofisi hiyo kwa mafunzo mazuri ambayo yatasaidia kuongeza umakini katika utunzaji wa majengo ya ofisi hiyo na kuahidi kuchukua tahadhari zote zinazohusu kinga dhidi ya majanga ya moto.



Sehemu ya Watumishi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, wakifuatilia mafunzo kuhusu namna ya kuchukua tahadhari dhidi ya majanga ya moto yaliyofanyika katika ofisi hiyo iliyopo Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma.



Afisa Tawala Mwandamizi, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. George Ndatta akifanya zoezi kwa vitendo la kuzima moto kwa kutumia gesi ya ukaa wakati wa mafunzo ya kuwajengea uelewa kuhusu tahadhari dhidi ya majanga ya moto kwa watumishi hao yaliyofanyika Mtumba jijini Dodoma.

11

NAIBU KATIBU MKUU, DAUDI ATAJA SABABU ZA WANACHI KUTOKUTUMIA MFUMO RASMI WA KUWASILISHA MALALAMIKO SERIKALINI

Na Lusungu Helela - DODOMA

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bw. Xavier Daudi amesema Wananchi walio wengi wamekuwa wakitumia mitandao ya Kijamii kufikisha malalamiko yao kwenye Taasisi za Serikali kutokana na baadhi ya Watumishi wa Umma kuvujisha siri za wateja wao pindi wananchi hao wanapotumia mifumo rasmi kutoa mrejesho

Amesema vitendo hivyo vimekuwa vikiwakatisha tamaa Wananchi wenye nia njema ya kuona Serikali inakuwa kinara wa kutoa huduma bora kwa wananchi wake.

Bw. Daudi ametoa kauli hiyo leo hivi karibuni jijini Dodoma wakati akifungua mafunzo maalum ya siku tatu kwa Maafisa Mrejesho kuhusu uendeshaji wa mfumo wa e-Mrejesho katika Ofisi za Umma.

Amewataka Maafisa hao kutunza siri za wateja wao ili kuwafanya Wananchi kuwa huru kuwasilisha changamoto zinazowakabili wakati wowote na mahali popote pasipo kulazimika kutumia mitandao ya kijamii

Bw. Daudi ameongeza kuwa Mfumo wa e-Mrejesho unampa fursa mwananchi kutuma malalamiko, pongezi pamoja na maulizo kwa Serikali mahali popote na wakati wowote.

Kufuatia hatua hiyo Bw. Daudi amewataka Maafisa hao mara baada ya kurudi katika vituo vyao vya kazi wakahakikishe wanakuwa waadilifu na wenye kutunza siri za ofisi na za wateja wao ili kuwafanya wananchi kuwasilisha malalamiko yao kwenye njia rasmi.

Aidha, Bw. Daudi amewataka Maafisa hao wakaimarishe Madawati au Ofisi za Mrejesho zilizopo katika Taasisi zao ili kufanikisha ushughulikiaji mrejesho kwa ufanisi na kwa wakati katika Ofisi za Umma kwa vile wameaminiwa kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Usimamizi wa Utawala Bora kutoka USAID/PS3+ awamu ya pili Dkt. Emmanuel Malangalila amesema wataendelea kushirikiana na Serikali ya Tanzania katika kuhakikisha mfumo huo unatumika ipasavyo katika Serikali za Mitaa ambako ndiko kuna malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi.

Mafunzo haya yanalenga kuona huduma zinazotolewa na Serikali zinafurahiwa na wananchi wote bila kujali rangi, kabila, mahali au hali yao ya kiuchumi waliyonayo amesisitiza Dkt. Malangalila.


Hivi karibuni Tanzania ilipewa tuzo ya Kimataifa ya ubunifu wa mfumo ya kidijitali wa Mrejesho (e-Mrejesho) nchini Korea Kusini na Shirika la Umoja wa Mataifa (UN) wakati wa Mkutano wa Umoja wa Jukwaa la Umoja wa Mataifa la Tuzo za Utumishi wa Umma (2024 UN Public Service Awards (UNPSF) kutokana na umadhubuti wake.



Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bw. Xavier Daudi akiwa kwenye picha ya pamoja na Maafisa Mrejesho mara baada ya kufungua mafunzo maalum ya siku tatu kwa Maafisa hao kuhusu uendeshaji wa mfumo wa e-Mrejesho katika Ofisi za Umma

Mrejesho

12 NENDENI MKALETE MAPINDUZI KATIKA MADAWATI YA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO YA WANANCHI - MKURUGENZI LEILA MAVIKA



Mwakilishi wa Katibu Mkuu, UTUMISHI, Bi.Leila Mavika akizungumza na Waratibu wa Kushughulikia Mrejesho jijini Dodoma wakati akifunga mafunzo maalum yaliyofanyika kwa muda wa siku tatu kwa Waratibu hao kuhusu uendeshaji wa mfumo wa e-Mrejesho katika Ofisi za Umma

Na Lusungu Helela - Dodoma

Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, UTUMISHI, Bi. Leila Mavika amewataka Waratibu wa Kushughulikia Mrejesho wakayatumie mafunzo waliyoyapata kuleta mapinduzi katika Madawati au Ofisi za Mrejesho zilizopo katika Taasisi zao ili kufanikisha ushughulikiaji mrejesho kwa ufanisi na kwa wakati katika Ofisi za Umma kwa vile wameaminiwa kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi.

Amewataka wakawe waaminifu na wenye haiba inayokubalika na Wateja wa ndani na nje ya Taasisi ili kuwafanya Wateja wao kuwa huru kufikisha malalamiko yao bila ya kuwa na wasiwasi wa aina yeyote.

Bi. Mavika ametoa kauli hiyo hivi karibuni Dodoma wakati akifunga mafunzo maalum yaliyofanyika kwa muda wa siku tatu kwa Waratibu wa Kushughulikia Mrejesho kuhusu uendeshaji wa mfumo wa e-Mrejesho katika Ofisi za Umma.

Bi.Mavika mewataka Waratibu hao kutoa fursa sawa kwa wananchi wote kwa kutumia mfumo wa e-Mrejesho ili kuwawezesha wateja kutuma malalamiko, pongezi pamoja na maulizo kwa Serikali mahali popote na wakati wowote.

Aidha, Mwakilishi huyo wa Katibu Mkuu,UTUMISHI, Bi.Mavika amewaonya Waratibu hao kuacha tabia ya kushughulikia mrejesho wa wananchi mara tu wanaposikia kuna ukaguzi maalum kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

"Nendeni mkawe kioo fanyeni kazi muda wote, hatutegemei kuona mnashughulikia mrejesho kutoka wananchi mara tu mnaposikia kuna ukaguzi maalum" amesisitiza Bi.Mavika.

Awali Kaimu Mkurugenzi wa Usimamizi wa Maadili, Bi. Janeth Mishinga ameeleza kuwa licha ya Waratibu hao kupewa mafunzo hayo ya kushughulikia mrejesho kwa wananchi kwa wakati pia wamepewa mafunzo ya mbalimbali ya kuwafanya kuwa Watumishi wa mfano katika jamii

Naye Mwenyekiti wa Waratibu wa kushughulikia Mrejesho, Denis Gondwe akizungumza kwa niaba ya Waratibu hao amesema mafunzo hayo yamekuwa ni muhimu sana kwao ikizingatiwa kuwa shabaha ya Serikali ya awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Rais Mhe.Dkt.Samia Suluhu Hassan ni kutoa huduma bora kwa wananchi wote bila ubaguzi wa aina yoyote.



Kaimu Mkurugenzi wa Usimamizi wa Maadili, Bi. Janeth Mishinga akizungumza na Maafisa Mrejesho jijini Dodoma kabla ya kumkaribisha Mwakilishi wa Katibu Mkuu, UTUMISHI, Bi.Leila Mavika kufunga mafunzo maalum ya siku tatu kwa Waratibu hao kuhusu uendeshaji wa mfumo wa e-Mrejesho katika Ofisi za Umma

13 WAZIRI SIMBACHAWENE ATOA MAAGIZO KUMI YA KIMKAKATI KWA WAKUU WA IDARA ZA UTAWALA NA USIMAMIZI WA RASILIMALIWATU SERIKALINI



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene ametoa maagizo 10 kwa Wakuu wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu Serikalini.

Maagizo hayo ni pamoja na kuzitaka Mamlaka za nidhamu kuchukua hatua stahiki na kwa wakati kwa watumishi wote waliobainika kuwa na barua za kughushi na walioshiriki katika mchakato wa kughushi barua za uhamisho kwa tarehe zilizobainishwa katika barua za maelekezo ikiwa ni pamoja na Waajiri kuacha kuwasilisha na kupitisha barua za maombi ya masuala mbalimbali ya kiutumishi ambayo kwa sasa yanashughulikiwa kupitia Mifumo.

Waziri Simbachawene, ametoa maagizo hayo hivi karibuni jijini Dodoma wakati akifungua kikao cha kazi cha siku tatu kwa Wakuu wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu chenye lengo la kuboresha utendaji kazi kwa Watumishi wa Umma Serikalini.

Amesema kwa nafasi walizonazo Wakurugenzi hao kwenye Taasisi wanazotoka ni jicho la Ofisi anayoingoza katika kusimamia utekelezaji wa Sera za Utawala, Maadili, Serikali Mtandao, Makazi ya Watumishi wa Umma, Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa na Usimamizi wa Rasilimaliwatu.

"Katika kutekeleza Sera tajwa hapo juu, mnawajibika kusimamia ukamilishaji wa taratibu za Ajira, mipango ya rasilimaliwatu, utendaji kazi, uendelezaji wa rasilimaliwatu na mifumo mbalimbali ya kiutumishi ambayo imesanifiwa kwa ajili ya kuwawezesha kutekeleza majukumu yenu. Mifumo hiyo ni pamoja na Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (e-Watumishi),

Pia Mfumo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma (ess) ambao una madirisha muhimu ya e-Utendaji, e-Uhamisho, e-Mikopo na e-Likizo. Vilevile, Mhe. Simbachawene amewafahamisha kuwa wana jukumu la kusimamia Maadili, nidhamu, utekelezaji wa Miundo na Mifumo ya uendeshaji wa utoaji huduma ili kuwa na Utumishi wa Umma wenye tija.

Katika agizo lake la pili Waziri Simbachawene amemuagiza Katibu Mkuu, UTUMISHI kutoendelea kufanyia kazi maombi yote yanayowasilishwa katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora nje ya Mifumo iliyoanza kufanya kazi ili kuhakikisha Mifumo hiyo inatumika ipasavyo.

"Agizo langu la Tatu, nawaelekeza Waajiri wote kuhakikisha mnajiunga na kutumia kikamilifu Mifumo ya Kiutumishi na Uwajibikaji ambayo imesanifiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuzinduliwa na Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa mnamo tarehe 23 Juni, 2024," amesema Mhe. Simbachawene.

Waziri Simbachawene katika agizo lake la Nne amewataka waajiri wote kuhakikisha wanasafisha taarifa za watumishi zilizopo katika Mfumo Jumuishi wa taarifa za kiutumishi na mishahara (e-Watumishi) kwa ajili ya kuwezesha utoaji uamuzi sahihi wa masuala mbalimbali ya kiutumishi.



Baadhi ya Wakuu wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wakimsikiliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (hayupo pichani) wakati akifungua kikao kazi cha Viongozi hao kilichofanyika katika Ukumbi wa Dodoma Jiji uliopo Mji wa Serikali Mtumba. Wengine ni

"Agizo langu la Tano, nawataka Wakuu wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu wote mhakikishe mnasimamia utekelezaji wa Mifumo kwa kuzingatia maelekezo yanayotolewa mara kwa mara na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora," amesema Mhe. Simbachawene.

Mhe. Simbachawene katika agizo lake la Sita amewataka Waajiri kuwa wabunifu na kutafuta ufumbuzi ili mipango ya Taasisi zao isiathirike au kutotekelezwa kwa kisingizio cha kukosa fedha;

Pia, Waziri Simbachawene amewaagiza Waajiri hususani wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga nafasi za ajira mpya kwa kuzingatia maelekezo ya mwongozo wa maandalizi ya Ikama na Bajeti hususan kwenye maeneo ya rasilimaliwatu yenye upungufu mkubwa na ambayo ni kipaumbele ikiwa ni agizo lake la Saba.

Aidha katika agizo lake la nane, Mhe. Simbachawene amewaagiza Waajiri wote kuwapokea watumishi waliopangiwa vituo vya kazi au waliohamishiwa katika Taasisi zao pamoja na kuwachukuliwa hatua stahiki watumishi wenye utendaji kazi usioridhisha kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utumishi wa umma.

Waziri ametoa agizo la Tisa na la Kumi akiwataka Waajiri wote kushughulikia ujazaji wa nafasi za uongozi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu na kuwaandaa watumishi wao na mabadiliko kwa kuwaandalia mafunzo yenye kukidhi matarajio ya nchi yetu, pamoja na mazingira yanayotuzunguka ili wakabiliane na mabadiliko yanayoendelea kwa kasi na teknolojia.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Deus Sangu akitoa maelezo ya awali kabla ya kumkaribisha Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (hayupo pichani) kuzungumza na Wakuu wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu katika kikao kazi cha Viongozi hao kilichofanyika katika Ukumbi wa Dodoma Jiji uliopo Mji wa Serikali



Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi akitoa utambulisho wa Viongozi waliohudhuria kikao kazi cha Wakuu wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu (hawapo pichani) kilichofanyika katika Ukumbi wa Dodoma Jiji uliopo Mji wa Serikali Mtumba.



Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Utumishi wa Umma, Bi. Felista Shuli akielezea malengo ya kikao kazi cha Wakuu wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu kabla ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (hayupo pichani) kufungua Kikao kazi hicho kilichofanyika katika Ukumbi wa Dodoma Jiji



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene akiwa katika picha ya pamoja na Wakurugenzi wa Idara na Vitengo wa ofisi hiyo mara baada ya kufungua kikao kazi cha Wakuu wa Idara za Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu kilichofanyika katika Ukumbi wa Dodoma Jiji uliopo Mji wa Serikali Mtumba. Wengine ni Viongozi mbalimbali waliohudhuria



Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-UTUMISHI, Bw. Juma Mkomi (wa kwanza kushoto) akizungumza wakati wa kikao kilicholenga kuimarisha ushirikiano katika Sekta ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kati ya ofisi hiyo na Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (SMZ) kilichofanyika jijini Dodoma.



Mkurugenzi wa Idara ya Mipango, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Bw. Cosmas Ngangaji (aliyesimama) akifafanua jambo wakati akiwasilisha mada kuhusu namna ya kuandaa mpango na bajeti wakati wa kikao kazi cha kuwajengea uwezo Maafisa Bajeti wa Ofisi hiyo kilichofanyika mkoani Manyara.



IMEANDALIWA NA

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi
wa Umma na Utawala Bora

Machi 2025